# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 34 Maombi

**SOMA Mhubiri 5:2; Waebrania 10:19 – 22 & 11:6; Yohana 15:7; Zaburi 66:18; Mathayo 6:9 – 13 & 7:7 & 11; Warumi 8:28; Marko 11:25 – 26; Mithali 15:29**

**SOMO**

Neno maombi katika Agano Jipya ni kuwazilisha haja zetu kwa mtu. Tukiomba Mungu inatakiwa tuwazilishe haja za moyo wetu zote Kwake. Lazima kwanza ndani yetu tujue tu wenye dhambi na tutake Mungu atusamehe ili tuwazilishe haja zetu. Na haja yetu kuu, tutamani Ufalme wa Mungu.

Maombi ni baraka kubwa sana yenye tuko nayo. Mungu ni muumba wa kila kitu lakini tukizungumza naye, huwa anatusikiliza. Tunaweza kuzungumza na Mungu wakati wowote, mahali popote lakini tusisahau kwamba tuko tunazungumza na muumba mkuu. Sisi ni wamoja baadhi ya viumbe vyake vingi. Lazima tuombe kwa unyenyekevu na heshima. Sulemani alisema, "Usiseme maneno ya ujinga kwa kinywa chako, wala moyo wako usiwe na haraka kunena mbele za Mungu. Mungu yuko mbinguni na wewe uko chini, kwa hivyo maneno yako yawe machache." (Mhubiri 5:2).

Tukielezea Mungu mawazo na hisia zetu ni njia moja ya uhusiano na Mungu. Mungu anataka sana kutusikia kwa hivyo inatupasa tuombe kila wakati kwa ajili ni ya maana kwa maisha yetu. Mazungumzo ni jambo la maana kwa uhusiano wowote. Inabidi tuwe na bidii. Tujue kwamba Mungu huwa anasikia maombi yetu.

Tukiomba Mungu, lazima tuamini kwamba anatusikia na atajibu maombi yetu. "Bila imani haiwezekani kumpendeza Mungu, kwa maana amwendeaye lazima aamini kwamba Yeye yuko na anawapa thawabu
wale wamtafutao." (Waebrania 11:6).

Yesu aliomba Baba yake kwa masaa nyigi. Wakati mwingine aliomba usiku kucha. Yesu alifundisha wanafunzi wake mfano wa sala - 'sala ya Bwana'. Hii sala inatuonyesha mambo ya muhimu yenye tunasitahili kuomba. Inaanza na kumsifu Mungu. Kumsifu Mungu inatakiwa iwe moyoni mwetu kila mara. Hii sala tunaomba Ufalme wa Mungu uje, hii iwe hitaji letu kubwa. Inasema tuombe juu ya nini tunachotaka cha msingi. Tuombe msamaha – lakini kama nasi tumesamehe wenzetu. Inazungumzia kuomba juu ya maisha yetu tukiendelea kwa safari ya kwenda kwa Ufalme. Inamaliza na sifa na utukufu kwa Mungu.

Maombi ni jambo la maana sana kwa maisha yetu. Kama nia yetu iko sawa, Mungu atatusikiliza. Mungu atatupa kilicho kizuri kwa kutuandalia twende kwa maisha ya milele kwa Ufalme Wake ujao. Lazima tusome neno lake ili tujue mengi kuhusu Mungu na kusudi Lake. Tuwe na maombi mafupi tukisifu na kushukuru Mungu. Tuombe msamaha tukimuuliza atusaidia na matakwa katika maisha ya saa hii. Hebu maombi yetu ituelekeze na tuwe na uhusiano mzuri na Mungu tukisafiri kuelekea kwa Ufalme wa Mungu.

### Maswali na Majibu

1. Mbona tuombe kwa unyenyekevu na heshima?
   *Kwa sababu Mungu ni Mkuu na muumba wa kila kitu*.
2. Sala ya Bwana inatufundisha tukiomba tuweke maneno gani?
   *Tuombe tukisifu Mungu, tuombe Ufalme uje, haja zetu, msamaha, atuelekeze kwa njia nzuri, tusifu na tushukuru.*
3. Mpatanishi ni nani?
   *Mtu anayechukua ujumbe kutoka kwa mmoja hadi kwa mwingine.*
4. Mbona tunaomba kupitia kwa Yesu?
   *Kifo cha Yesu kilifungua njia ya kwenda kwa Mungu. Yeye ndiye anatupelekea maombi kwa Mungu.*
5. Inajalisha vile tunaomba ama wapi? *Hapana, Mungu anajali tunayoyasema.*
6. Mungu huwa anajibu maombi yetu?
   *Mungu anajibu maombi yetu vile anaona na kwa uzuri wa milele.*
7. Mbona tuombe hivi 'Kama ni mapenzi Yako.'
   *Tunatakiwa tutake kuwa kwa Ufalme Wake sana, kwa hivyo tukubali kwamba Mungu anatutakia mazuri.*
8. Mungu alijibu Yesu namna gani alipoomba kwamba asiteswe msalabani?
   *Mungu hakumhebesha hayo mateso, lakini alimpa nguvu ya kuistahimili.*
9. Majibu matatu yenye Mungu huwa anatupa ni gani? *Ndiyo. Hapana. Ngoja.*
10. Kama inaonekana Mungu hajatujibu, tubadilishe na tuombe namna gani?
    *Omba kwamba iwe mapenzi yake, omba kila mara, omba msamaha, kuwa na subira, fikiria labda Mungu amekujibu kwa njia nyingine, na tuajibike.*

**Mistari ya kukariri** Zaburi 37:4 Mhubiri 5:2 Warumi 8:28 Waebrania 10:19 – 22

### Mazungumzo

Tunatakiwa tuombe nini? Kunayo vitu vyenye hatutakiwi kuomba? Maombi yanaweza kubadilisha maisha yetu namna gani?

### Kuandika

Luka 6:28; Wakolosai 4:3; Yakobo 5:16 – 18; Ayubu 42:8. Hizi mistari zinatufundisha tuombee nani. Andika orodha ya watu wenye utaombea juma ijao.

Kwa Agano la Kale watu walikuwa wakichinja mnyama kama dhabihu ili wasamehewe dhambi zao. Watu walikuja kwa Mungu kupitia kwa makuhani. Yesu alipotoa mwili wake usio kuwa na mawaa kupitia kwa kifo, pasia ya hekalu iliraruka kwa vipande viwili. Hii ilimaanisha njia ya kwenda kwa Mungu imefunguliwa. Yesu alitufungulia njia ya kwenda kwa Mungu. (Waebrania 10:19 – 22). Kupitia kwa kifo cha Yesu ndiyo dhambi zetu zinaweza kusamehewa. Yesu ni mpatanishi. Mpatanishi ni mtu anayechukuwa ujumbe kutoka kwa mtu mmoja hati kwa mwingine. Mungu ni mtakatifu na mnyofu sana hata hatuwezi kumfikia wasi wasi. Yesu anatuazilisia maombi yetu kwa Mungu na kututetea. Maombi yetu lazima iende kupitia kwa Yesu. Yeye anayawazilisha kwa Mungu.

Tunatakiwa tuombe namna gani na tukiwa wapi? Eliya alifunga mlango akiomba, Petro aliomba akiwa kwa paa ya nyumba, Nehemia aliomba kimoyo moyo akiwa mbele ya mfalme, Danieli aliomba akiwa ameangalia Yerusalemu, Kornelio aliomba usiku wa manane, Eliya aliomba kama ameweka kichwa chake katikati ya magoti yake, Daudi alikaa mbele ya Bwana, Sulemani aliinua mikono yake juu kuelekeza mbinguni. Hizi mifano kutoka kwa Biblia inatuonyesha kwamba tunaweza kuomba Mungu mahali popote, wakati wowote na juu ya jambo lolote. Mungu anajali kwamba tunasema nini sio kwamba tuko wapi au ni wakati gani. Tukiomba na nia sahihi, wakati wote Mungu atatusikia.

Maombi si lazima ichukuwe muda mrefu. Lakini ni vyema kuwa na wakati na Mungu kila siku kuonyesha uhusiano mzuri kati yako na Mungu. Tunatakiwa tuwe na wakati tukikusanya mawazo yetu juu ya Mungu kwa maombi. Kila siku tunatakiwa tufikirie kwa umakini kabla ya kuomba na tunaomba juu ya nini. Si vyema kila wakati tuseme maneno yale yale tunapoomba bila kufikiria. Tufikirie sana kabla ya kuanza kuomba. Tunaweza kuwa na orodha ya watu au mambo yenye tunatakiwa tuombee. Lazima tuwe na uhaki ya maombi yetu. Tusiwe wachoyo kwa kujiombea sisi wenyewe tu. Tukiomba kwamba Mungu atusaidie tushinde dhambi zetu, tujaribu kwa hiyo siku tusitende dhambi hiyo hiyo. Tuwe tayari kusikiliza na kungojea Mungu atujibu hayo maombi.

Tunatakiwa tuombe juu ya nini? Yesu alisema, “Omba na utapewa; tafuta na utapata; bisha na utafunguliwa mlango. “Ikiwa nyinyi ….mnajua kuwapa watoto wenu zawadi nzuri, si zaidi Baba wenu wa mbinguni kuwapa zawadi nzuri wale wanaomuomba!” (Mathayo 7:7 & 11) na “ Mkibaki ndani yangu na maneno yangu yabaki ndani yenu, ombani lolote mtakalo, na mtapewa.” (Yohana 15:7). Mungu ni Baba wetu na anatujali kama baba anajali mtoto wake.

Biblia inatupa mifano ya watu wakiomba juu ya nini: Paulo aliombea watu kukua kiroho, Danieli alishukuru Mungu mara tatu kwa siku, Wakristo waliombea Petro alipokuwa gerezani, Yesu aliomba Mungu alinde wanafunzi wake, Paulo aliomba ‘mwiba mwilini’ (labda ugonjwa au kutoona vizuri) umwondokee, Hana aliomba apate mwana.

Mungu hatatupea kila kitu tunachoomba. Tukiomba na nia nzuri, Mungu atasikiliza maombi yetu. Atajibu vile anaona ni vyema kwetu. Mungu hajatuahidi kwamba atatuondolea shida zote zenye tuko nazo na kutupea kila kitu tunachotaka. Paulo anatwambia, “Twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao kuwapa mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake”. (Warumi 8:28). Mungu anataka tuwe kwa Ufalme Wake na wokovu wetu ndio kitu **kizuri** amewaihidi wale walio na imani. Chochote kinachofanyika kwetu sasa, ni Mungu anafanya kwa faida yetu. Mungu hujibu maombi yetu kwa namna ya kututayarisha kwa Ufalme Wake ujao.

Wakati mwingine wazazi wetu hawatupei kila kitu tunachotaka. Wazazi wetu wanajua nini kinachotufaa. Si vizuri sisi kupewa kila kitu tunachotaka. Tunaweza kukasirikia wazazi, lakini tukikua wakubwa tutajua kwamba walikuwa haki. Si halisi zaidi basi, Mungu kujua kinachotufaa! Inatupasa tuombe kila wakati namna hii, “Kama ni mpenzi Yako.” Tutake sana kuwa kwa Ufalme na tujue Mungu anajua kilicho bora kwetu.

Katika bustani ya Gethsemane Yesu aliomba kwamba asiumie na afe msalabani. Kama hayo maombi yangejibiwa, hatungekuwa na tumaini la wokovu. Lakini Yesu aliomba, “Mapenzi yako yatimizwe”. Mungu alisikia na kujibu maombi ya Yesu. Mungu hakuondoa mateso ya msalaba lakini alisaidia Yesu nguvu ya kuisitahimili.

Mungu huwa anasikia maombi yetu. Wakati mwingine jibu ni ndiyo, wakati mwingine ni hapana, na wakati mwingine, ongoja. Tukiona Mungu hajibu maombi yetu, tusikufe moyo. Labda tunatakiwa tuombe tofauti. Labda chenye tunataka si mapenzi ya Mungu. Labda hatuombi kila siku. Labda hatujatubu dhambi zetu na ndio zinakuwa kipingamizi kwa maombi yetu. (Zaburi 66:18; Mithali 15:29; Marko 11:25 – 26). Labda hatuna uvumilivu wa kuongoja jibu la Mungu. Labda Mungu ametupea jibu tofauti na vile tulitarajia. Labda nasi tunajambo la kufanya kabla. Kwa mfano, kama mwanafunzi anataka apite mtihani na hali hana haja na kufunzwa au kusoma, Mungu hatajibu hayo maombi.

⇨